



Wapenzi Jamii za Shule za Umma za Kata ya Fayette:

Wilaya yetu ya shule imeazimia kutoa elimu ya hali bora kabisa kadri ya uwezo wetu kwa kila mwanafunzi, bila kujali kiwango cha mapato ya jamii yake. Ili kuhakikisha kwamba shida za kifedha si kizuizi, wanafunzi watakaofuzu kupata chakula bila kulipa au kwa gharama iliyopunguzwa kutokana na udhibitishaji wa moja kwa moja au kutoka vielekezo vya mapato pia wameondolewa kutoka malipo ya ufundishaji kama:

1. Malipo au fedha zinazochukuliwa na shule kugharamia matumizi ya mali ya shule, pamoja na lakini sio hizi pekee: vifuli (locks), tauro, vyombo vya maabara, na vitabu spesheli vya kuandikia.
2. Malipo ya kuenda ziara, ambayo sehemu yake fulani itakuwa ndani ndani ya wakati siku ya shule.
3. Malipo au fedha zilizochukuliwa kugharamia nguo za shule au vifaa vinavyohusiana na michezo ya vikundi fulanii shuleni, muziki, au mipango ya sanaa za makini (fine arts).
4. Vifaa spesheli au malipo yanayohitajika kwa darasa fulani.
5. Malipo ya kuhitimu yanayohitajika ili kushiriki.
6. Malipo ya elimu spesheli.
7. Malipo ya rekodi za shule.
8. Malipo ya huduma za afya za shule.
9. Malipo ya shughuli za jumla.
10. Malipo ya masomo ya kikazi.
11. Malipo ya kukodisha vitabu vya kusoma.
12. Malipo mengine yoyote ambayo hayajaondolewa kwa mujibu ya kanuni za bodi ya shule au taratibu.

Ili kutuma ombi la kuondolewa kwa malipo, tafadhali jaza, weka sahihi kwa ombi, na mrudishe karatasi iliyojazwankwa ofisi ya mwalimu mkuu wa shule ya mtoto wako.

Ahsante kwa kutilia hili swala maanani. Ukiwa na maswali yoyote ya ziada, tafadhali wasiliana na mwalimu mkuu wa shule ya mwanao.

FOMU YA KUOMBA KUSAMEHEWA MALIPO YA KIMASOMO

TAFADHALI RUDISHA HII FOMU KWA OFISI YA SHULE YA MTOTO WAKO

M/wanafunzi a/wafuatao wa shule ya _____ a/wanaishi nyumbani kwangu na a/wamefuzu kupata chakula cha mcana bila malipo ua kwa gharama iliyopunguzwa na ninaomba a/wasamehewe kulipa malipo ya kimasomo.

Nimeipatia Ofisi ya Lisho la Watoto ya FCPS kumpasha mfanyikazi wa shule anayehusika na hili jambo na mwalimu wake habari kuhusu hali ya chakula ya mtoto wangu ili mtoto wangu aweze kunufaika kutokana na fedha za Usamehewaji wa Malipo (Fee-Waiver funds).

Jina la Mwanafunzi	Tarehe ya Kuzaliwa	Darasa

Sahihi ya Mzazi/Msimamizi _____

Jina la Mwanafunzi _____ Tarehe _____

.....

FOMU YA KUJIONDOA KWA HIARI KUSAMEHEWA MALIPO YA KIMASOMO

Ninaelewa kwamba, kama mtoto wangu atafuzu kuweza kusamehewa malipo ya kimasomo na nimetia sahihi na kuirudisha Fomu ya Kuomba Kusamehewa Malipo, SITARAJIWI kulipa, kuchangia au kutoa sehemu yoyote ya malipo halali ya shule (pamoja na malipo yanayogharamia malipo ya ziara wakati wa shule). Hata hivyo, nikitia sahihi kwa hii fomu ya kujiondoa, ninachagua, kutoka mara kwa mara, kulipa yote au sehemu ya hizi gharama. Ili kuweza kutoa mchango wa hiari, ni lazima nisahihishe hii fomu.

Sahihi ya Mzazi/Msimamizi _____

Jina la Mwanafunzi _____ Tarehe _____

MATUMIZI YA SHULE PEKEE

Ombi lako la kusamehewa malipo ya kimasomo kumhusu _____

___ Limekubaliwa

___ Limekataliwa kwa sababu ya _____

Kama ombi lako limekataliwa na ungetaka kuongea kuhusu huu uamuzi, unaweza kumpigia simu _____ kuomba mkutano.

Mwalimu Mkuu au Mwakilishi

Tarehe